

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO

IAA SACCOS LTD



SERA YA AKIBA, HISA NA AMANA

PRI-ARS-2022-855

OKTOBA 2024


SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI

1.1. HISTORIA YA CHAMA:-

IAA SACCOS LTD ilisajiliwa tarehe 27 Mei 2003 ikiwa na wanachama 36 na hisa zenye thamani ya Tshs. 1,800,000/= (Milioni moja na laki nane tu). Thamani ya Hisa imekuwa ikiongezeka Mwaka hadi Mwaka ambapo kufikia Tshs. 50,000/= (Elfu hamsini tu) Chama kina Hisa zenye thamani ya Tshs. 8,300,000/= (Milioni nane laki tatu).

Ongezeko la thamani za Hisa limechangiwa na kuongezeka kwa wanachama wa IAA SACCOS LTD. Hata hivyo, ongezeko la Wanachama limesababisha kuwepo kwa changamoto ya utoaji huduma iliyo bora na hivyo Chama kulazimika kuwa na Sera na Miongozo mbalimbali itakayosaidia utoaji wa huduma bora kwa manufaa ya Chama na wanachama wenyewe.



1.2. Madhumuni ya Chama:-

Madhumuni ya IAA SACCOS LTD, ni kuinua na kuimarisha hali ya wanachama wake kiuchumi na kijamii. Ili kufikia lengo Chama kitafanya shughuli zifuatazo:-

- a) Kupokea Hisa na Akiba za wanachama na kuzihifadhi kwa njia rahisi na salama
- b) Kutoa mikopo ya huduma za kijamii na kiuzalishaji yenye masharti nafuu
- c) Kuelimisha wanachama kujijengea tabia ya kuweka Akiba na Amana na kutumia kwa busara mikopo watakayokopeshwa na Chama.
- d) Kutoa faida juu ya Akiba za wanachama.
- e) Kuhamasisha wananchi wengine wasio wanachama kujiunga na Chama kwa kuzingatia Sera na Masharti ya Chama.

1.3. Mikakati ya jumla ya Chama:-

Mikakati ya jumla ya Chama kwa miaka 5 ijayo, kuanzia mwaka 2020 mpaka 2024 ni kama ifuatavyo:-

- a) Kutumia fursa zilizopo kupanua vyanzo vya huduma ya kifedha na kuhamasisha wanachama kuweka Hisa na Akiba ili ziweze kujenga mtaji wa uhakika wa ndani wa kukopeshana.
- b) Chama kinaamini kuwa upanuzi wa vyanzo vya fedha utawezesha :-
 - i. Kuondoa foleni ya maombi ya mikopo
 - ii. Kutoa mikopo ya aina mbalimbali kwa wanachama
 - iii. Kutoa gawio juu ya Akiba
 - iv. Kuvutia wasio wanachama kujiunga na kuwekeza kwenye Chama

1.4. Dira:-

IAA SACCOS LTD inadhamiria kuwa SACCOS bora katika Mkoa wa ARUSHA inayojitegemea kwa mtaji wa ndani, kuboresha maisha ya wanachama wake ili kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2024.

1.5. Mwelekeo:-

IAA SACCOS LTD itatoa huduma bora na mikopo yenye masharti nafuu kwa wanachama wake, kuwajengea uwezo wa mtaji na stadi za biashara kwa njia endelevu.

1.6. Amali:-

Ili kuweza kufikia dira iliyojiwekea kwa miaka 5, IAA SACCOS LTD inaamini juu ya mihimili ifuatayo:-

- i. Uadilifu wa Wanachama, Viongozi na Watumishi.
- ii. Kuendesha shughuli za Chama kwa kuzingatia demokrasia ya kweli.
- iii. Usawa wa jinsia.
- iv. Uwazi na ukweli.
- v. Utawala wa Sheria.
- vi. Upendo.
- vii. Uwajibikaji.

SEHEMU YA PILI

2. SERA YA UHAMASISHAJI WA HISA, AKIBA, NA AMANA

2.1. Madhumuni ya Sera:-

Madhumuni makuu ya Sera hii ni kuwa na mfumo bora wa utoaji huduma kwa wanachama kwa lengo la kuinua kipato cha Chama na Wanachama wake, kupanua wigo wa biashara ya kifedha ili kukiwezesha Chama kuwa na misingi endelevu na ya kiujasiriamali katika kuendesha shughuli za Chama kwa faida.

Aidha Chama kinahitaji mfumo madhubuti wa Hisa, Akiba, Amana ili kukabiliana na matukio yafuatayo:-

- a) Kupungukiwa au kutokuwa na fedha/mtaji wa kukopesha Wanachama wake.
- b) Kutokutekelezwa kwa maelekezo na malengo yaliyoainishwa katika Masharti, Mpango Biashara na Maamuzi ya Wanachama.
- c) Kutoa mikopo bila utaratibu, na hivyo kutorejeshwa kwa mikopo kwa wakati au kuwepo kwa mikopo hewa.
- d) Hatari zitokanazo na:-
 - i. Uzembe wa Wanachama, Viongozi na Watumishi.
 - ii. Makosa mengine ya kibinadamu.
 - iii. Hila na ulaghai wa aidha Wanachama au Viongozi au Watumishi wasio waadilifu.

Kwa kuwa na mfumo mzuri na kuutekeleza utakidhi mambo yafuatayo ndani ya Chama:-

- a) Itawapa Uongozi na Watumishi wa IAA SACCOS Ltd. utaratibu wenye mantiki, kama nyenzo ya kuendesha shughuli za Chama za kila siku.
- b) Sera ni nyenzo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Chama kwa kuzingatia misingi ya utawala bora:-
 - i. Uadilifu
 - ii. Uwajibikaji
 - iii. Uwazi na Ukweli
 - iv. Utawala wa Sheria
 - v. Usawa na Demokrasia
- c) Kutumia fursa zinazozunguka katika mazingira ya nje ya Chama ili kutoa bidhaa na huduma zitakazokuwa chachu kwa wanachama na wateja kuwekeza zaidi katika Chama kwa lengo la kujenga mtaji imara wa ndani wa kukopeshana, mtaji ambao utakiwezesha Chama kama ifuatavyo:-
 - i. Kupunguza utegemezi wa mitaji ya nje/mikopo.
 - ii. Kutoa mikopo ya aina mbalimbali inayokidhi mahitaji halisi ya Wanachama.
 - iii. Kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo kwa Wanachama.
 - iv. Chama kuzalisha faida kutokana na shughuli zake ambazo zitakifanya Chama kiweze kutoa faida juu ya Akiba.
 - v. Kuwavutia wadau wengine wa Chama kuingia ubia na Chama na kushawishi wasio wanachama kujiunga na kuwekeza kwenye Chama.

2.2. Maana ya Sera ya Hisa, Akiba:-

Sera ya Hisa, Akiba, Amana na Mikopo ni mfumo na utaratibu wa Utawala katika Uwekaji na uchukuaaji wa Hisa, Akiba, Amana na udhibiti wa utoaji wa Mikopo na urejeshaji uliowekwa na Wanachama kwa madhumuni ya kuendesha shughuli za Chama kwa mantiki na mpangilio wenye ufanisi. Mfumo huu unaweka utaratibu wa Utawala wa kifedha na ule usiokuwa wa kifedha.

2.3. Maana ya Hisa, Akiba Amana:-

2.3.1. Hisa:-

Maana yake ni kiwango cha chini cha thamani ya hisa kinachotakiwa kulipwa na mwanachama kwa ajili ya uanachamani jumla ya hisa zote za uanachama na hisa za hiari.

2.3.2. Akiba:-

Maana yake ni fedha zinazoweza kuchukuliwa na mwanachama kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa katika masharti ya SACCOS; Akiba italipwa faida kwa kiwango kitakachowekwa na Mkutano Mkuu kila Chama kinapopata faida.

2.3.3 Amana

Maana yake ni fedha anazoweka mwanachama katika chama na anauwezo wa kuzichukua muda wowote anapohitaji.

Chama kitakuwa na amana za aina mbili

- i. Amana za kawaida
- ii. Amana za muda maalumu – Chama kitapokea Amana za muda maalumu kuanzia **mwaka mmoja** kama ifuatavyo;

SN	KIASI CHA AMANA	RIBA KWA MWAKA (5%)
1	5,000,000	250,000
2	10,000,000	500,000
3	15,000,000	750,000
4	20,000,000	1,000,000

SEHEMU YA TATU

3. KIWANGO CHA CHINI CHA HISA ZA UANACHAMA NA UWEPO WA HISA ZA HIARI.

- a) Kiwango cha hisa kwa kila mwanachama wa IAA SACCOS ni shilingi 50,000/- kwa hisa moja na kila mwanachama anatakiwa kuwa na Hisa 10 zenye thamani ya shilingi 500,000/-.
- b) Hisa za mwanachama hazitatumika kama dhamana ya mkopo.
- c) Mwanachama wa IAA Saccos anaweza kuweka HISA ZA HIARI ambazo anaweza kuzitumia kama dhamana ya mkopo.

SEHEMU YA NNE

4. MASHARTI YA UANACHAMA NA KUTOA HISA ZA HIARI NA AKIBA,

- a) Mwanachama wa IAA Saccos hataweza kutoa Hisa labda kama-;
 - i. Mwanachama ataacha uanachama au kufariki
 - ii. Taarifa za Hesabu ziwe zimekaguliwa na mkaguzi wa nje kwa mwaka husika au SACCOS iwe imelimbikiza faida kwa mwaka husika.
- b) Hisa za Hiari na Akiba za mwanachama zinaweza kuchukuliwa wakati wowote isipokuwa kama Hisa hizo za Hiari na Akiba hiyo imetumika kama dhamana ya mkopo wa mwanachama husika.
- c) Endapo mwanachama wa IAA Saccos anataka kupunguza akiba yake anatakiwa kupunguza kwa asilimia sitini (60%) ya Akiba zake aidha Hisa za Hiari au Akiba atatakiwa kutoa taarifa ya siku 14 kwa maandishi akieleza kusudio lake la kutoa kiasi hicho cha fedha.

Mwenyekiti wa Bodi

[Signature]

Katibu wa Chama

[Signature]

Mraji wa Vyama vya Ushirika

Robert R. George

Tarehe 10/12/2025

Asst. REGISTRAR OF CO-OPERATIVE SOCIETIES
ARUSHA